# Ukiushi wa 'Kanoni' ya Maudhui katika Fasihi ya Watoto ya Kiswahili

*Mutahi Miricho, Sheila Wandera-Simwa, Wendo Nabea*
**Laikipia University, Kenya**

## Abstract
*The objective of this paper is to bring out canon deviations in children's literature. In examining the deviations, this paper will specifically look at canon thematic deviation in the sense that the sampled stories have themes that in traditional canon were not included in children's literature such as themes on politics and crime investigation. Social realism theory will be used to evaluate canon deviation with a view of indicating that children's literature is not just about fantasy but it is based on real events in the writer's society. The paper highlights on new development in Kiswahili children's literature in Kenya. This will enlighten upcoming authors on how to create works on children's literature. At the same time when this deviation is highlighted it might give rise to scholarly debate on whether children's literature must stick to traditional canon or it could be written freely as per the writer's creativity.*

**Key words**: Canon, children's literature, deviations, politics, theme.

## Ikisiri
*Lengo la makala hii ni kubainisha ukiushi wa 'kanoni' katika fasihi ya watoto. Katika kuchunguza ukiushi huu, makala hii itajishughulisha na ukiushi wa 'kanoni' kimaudhui kwa maana kuwa hadithi zilizoteuliwa zimeshughulikia maudhui ambayo kidesturi hayakuwa yakishughulikiwa katika fasihi ya watoto. Maudhui hayo ni yale ya kisiasa na upelelezi. Nadharia ya uhalisia wa kijamaa itatumiwa kutathmini ukiushi wa 'kanoni' kimaudhui ili kuonyesha fasihi ya watoto si fantasia tu lakini ina msingi katika matukio halisi katika jamii ya mwaandishi. Makala hii inalenga kuangazia hatua mpya katika maendeleo ya fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya. Hii inaweza kuwapa mwangaza zaidi waandishi wapya wanaonuia kutunga fasihi ya watoto. Aidha, ukiushi huu ukidhihirika, unaweza kuzua mgogoro mpya kuhusu iwapo fasihi ya watoto izingatie 'kanoni' za kimapokeo au iandikwe kwa njia huru kulingana na ubunifu wa mwaandishi.*

**Maneno Muhimu:** Fasihi ya watoto, 'kanoni', maudhui, siasa, ukiushi.

## Utangulizi
Fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayolenga hadhira ya watoto. Kimsingi, huwa na dhima ya kuwaadilisha, kuwaburudisha na kuwafunza. Lengo la makala hii ni kubainisha ukiushi wa 'kanoni' ya maudhui katika fasihi ya watoto. Kidesturi, fasihi ya watoto imekuwa ikijihusisha na maudhui yanayohusu ujenzi wa maadili miongoni mwa watoto lakini katika karne ya ishirini fasihi hii yaelekea kubadilika na kuchukua mielekeo mipya kimaudhui kwa kuanza kupenyeza maudhui yenye itikadi za kisiasa. Vilevile, maudhui yanayohusu upelelezi yameanza kujipenyeza katika fasihi hii. Mabadiliko haya ndiyo yanayochukuliwa katika makala hii kama ukiushi wa kimaudhui. Ili kuchunguza ukiushi huu, makala hii itarejelea vitabu vitatu vya fasihi ya watoto. Vitabu hivyo ni *Sungura Mpanda Ngazi* na *Urembo wa Ngiri* vilivyoandikwa na John Kobia na kimoja kilichoandikwa na K.W. Wamitila ambacho ni *Kijana Mpelelezi*.

## Msingi wa Nadharia

Nadharia ya uhalisia wa kijamaa imetumiwa kutathminia maudhui ili kuhusisha matukio ya hadithi na matukio halisi ya kisiasa katika jamii na kuonyesha kuwa fasihi ya watoto si ya kifantasia tu kama inavyochukuliwa na watu wengi kama vile Wamitila (2008) anayedai kuwa fasihi ya watoto imejengwa katika misingi ya fantasia. Nadharia ya uhalisia iliwekewa misingi na mwanafalsafa G.F. Hegel (1770 – 1831) katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetics*. Hegel alipendekeza matumizi ya neno 'Uhalisia' kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawasilisha ulimwengu wa kijamii ambako kuna wahusika wa kawaida wanaotenda mambo ambayo yanaakisi hali halisi ya maisha yao ya kila siku. Mandhari na matukio ya kazi hizi huwa yale yanayowezekana wala si yale ya kidhahania. Nadharia ya uhalisia inatokana hasa na nadharia pana ya sosholojia ya fasihi hasa tukizingatia mawazo ya wataalamu wengine kama vile Taine na Georg Lukas. Kwa mujibu wa Swingerwood (1975), Taine alilinganisha fasihi na kioo na kueleza kuwa fasihi huakisi maisha ya jamii kama vile kioo kinavyoakisi sura ya mtu anayejitazama. Utafiti huu utaongozwa na mihimili mikuu ya nadharia ya uhalisia ambayo ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii na kuwepo kwa wahusika wanaotenda vitendo vinavyowakilisha matendo halisi ya watu wanaoweza kutambulika katika jamii ya mwaandishi. Matendo ya watoto ni tofauti na matendo ya watu wazima katika jamii na hivyo ikiwa kazi ya fasihi ya watoto imejikita katika matendo ya watu wazima kama vile siasa itakuwa na ukiushi wa kimaudhui.

## 'Kanoni' ya Maudhui ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayotungwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Fasihi ya watoto huandikwa na huhakikiwa kwa misingi ya kazi ambazo kidesturi zinatambuliwa kama 'kanoni' za vigezo vya kupimia ubora wa fasihi hii. 'kanoni' hizi zimekitwa katika sifa za fasihi ya watoto na imekuwa kama ni mwiko kuzikiuka sifa hizo. Mawazo ya wataalamu kama vile Hunt (2002) na Bhroin na Patricia (2012) yameweka msingi wa ni vipi fasihi ya watoto iandikwe. Wataalamu hao wametoa maoni kuhusu mambo yanayofaa na yasiyofaa kuambiwa watoto katika fasihi. Hunt (2002) anaeleza kuwa fasihi ya watoto imeelekea kuepuka masuala yanayohusu itikadi za kisiasa labda ikichukuliwa kuwa yanafaa kushughulikiwa tu katika fasihi ya watu wazima. Bhroin na Patricia (2012) wanajiuliza ni nini kinachofaa kuambiwa watoto. Hunt (2002) amedai kuwa fasihi ya watoto inapaswa kuthibitiwa na kuchuja mambo ambayo watoto huambiwa kupitia fasihi hii. Kutokana na maoni ya wataalamu hawa kuhusu kazi ya fasihi ya watoto iandikwe vipi, fasihi hii imekuwa ikizingatia kanuni fulani.

Laundin (2004) anazungumzia dhana ya 'kanoni' akisema ina mizizi yake katika Biblia na sheria za kidini. Anaeleza kuwa katika fasihi, 'kanoni' ina maana ya kazi za kifasihi, hasa za awali, zilizofana kiasi kwamba zinatumika kama vigezo vya kupimia kazi zingine za utanzu husika. Hivyo, ikiwa kazi haikuzingatia sifa sawa na kazi hizo, inasemwa kuwa imekiuka 'kanoni'. 'Kanoni' katika fasihi basi ni kama mkusanyiko wa vitabu ambao dhima yake kuu ni kuwa kigezo cha kulinganishia kazi na nyingine. Bakize (2014) anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayowahusu watu walio chini ya umri wa miaka kumi na minane. Ngugi (2012) naye anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Anaeleza kuwa fasihi hii huzingatia sifa maalumu zinazoibainisha. Kimaudhui, Bakize (2014) anaeleza kuwa maudhui ya hadithi za watoto huwalenga watoto. Wamitila (2016) anafafanua maudhui kama jumla ya mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Yaliyomo katika hadithi yanahitajika yamhusu na yalingane na tajriba ya mtoto ili aweze kufaidi kutokana na hadithi anayosoma. Watoto hufurahia wahusika mashujaa. Wao huvutiwa na hadithi ambapo mhusika anashinda hali ngumu inayomkabili. Hadithi kama hizo huwapa moyo na matumaini

kuwa hata na wao wanaweza kushinda changamoto zinazowakabili. Waandishi wa hadithi za watoto hujikita katika ulimwengu wa mtoto na kazi zao huhusu tajriba za watoto kama vile majukumu yao katika jamii, maadili na shughuli zao shuleni na nyumbani. Huwa na mada au wazo kuu linalolenga na linalowavutia watoto. Maudhui ya hadithi hizi ni rahisi kueleweka na watoto.

Bakize (2014) anaeleza kuwa mwega wa fasihi ya watoto ni watoto wenyewe moja kwa moja na hivyo, fasihi hii hujikita katika ulimwengu wa mtoto. Huzungumzia mambo ambayo mtoto anafanya, anayaona au anawaza. Bakize (2014) anaeleza kuwa kazi nyingi za fasihi ya watoto huwa na lengo la uadilishaji. Maudhui mengi ya hadithi za kiwango hiki yanahusu mandhari ya nyumbani na shuleni ambayo yanajulikana kwa watoto walengwa kama vile darasani, shuleni, nyumbani, familia, shambani, ndege na wanyama wa nyumbani, michezo, vyakula, mimea afya na usafi. Kutokana na utafiti kwa ajili ya makala hii, imebainika kuwa fasihi hii imekuwa ikijishughulisha na masuala ya maadili, wema, utiifu, jasira na vituko vya watoto huku ikichukuliwa kama kosa kuyashughulikia masuala ya ulimwengu wa watu wazima kama vile siasa, mapenzi na uchawi. Kwa mfano, katika mradi wa JKF wa *Adili* na mradi wa KLB wa *Nasaha Zetu* ambao chini yake hadithi nyingi za watoto zimechapishwa, neno 'adili' linaelekeza kwenye maudhui ya kuhimiza tabia njema. 'Nasaha' nalo linaelekeza kwenye maudhui ya maadili.

Kutokana na maelezo ya Ngugi (2012) na Hunt (2002), kazi za fasihi ya watoto katika Kiswahili ambazo zinaweza kuchukuliwa kama 'kanoni' ni zile za waandishi waliotangulia kuandikia utanzu na ambazo zaonekana kuweka msingi wa fasihi ya watoto. Kazi kama hizo kutoka nchini Kenya ni kama vile *Mtaka Yote Hukosa Yote* (Omolo, 1968), *Mikasa ya Joseph Juma* (Omolo, 1971), *Kuishi Kwingi ni Kuona Mengi* (Somba, 1968) na *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani* (Somba, 1969). Kazi hizi zilisomwa na waandishi waliofuatia na kwa muda mrefu zilikuwa kama 'kanoni' au vigezo vya fasihi ya watoto iandikwe vipi na ishughulikie masuala gani. Hata hivyo, hali hii imebadilika na fasihi ya watoto yaelekea kuchukua mielekeo mipya kimaudhui na kifani. Ukiushi wa 'kanoni' umeanza kujitokeza katika kiwango cha maudhui na kiwango cha fani hasa kutokana na baadhi ya waandishi wa fasihi ya watoto wa karne ya ishirini na moja. Makala hii inachunguza ukiushi wa 'kanoni' katika kiwango cha maudhui na kiwango cha fani kwa kurejelea kazi teule za fasihi ya watoto katika Kiswahili.

## Ukiushi wa 'Kanoni' Kimaudhui katika Fasihi ya Watoto

Utafiti wa makala hii umeonyesha kuwa katika miaka ya hivi karibuni, hasa katika karne hii ya ishirini na moja, wameibuka waandishi wa fasihi ya watoto wanaoelekea kukiuka 'kanoni' za fasihi ya watoto kwa kuingiza masuala halisi ya kisiasa na yale ya upelelezi. Waandishi hao ni kama vile John Kobia ambaye tangu mwaka wa 2007 ameanza kupenyeza maudhui ya siasa polepole katika kazi za watoto lakini kwa njia isiyo ya wazi. Mwingine ni Kyalo Wadi Wamitila ambaye ameingiza maudhui ya upelelezi katika fasihi ya watoto. Fasihi ya watoto yaelekea kukiuka 'kanoni' na kuchukua mielekeo mipya kimaudhui na kifani. Itikadi za kisiasa, zilizochukuliwa kama zinazofaa kushughulikiwa tu katika fasihi ya watu wazima, zinaanza kujipenyeza katika hadithi za watoto. Maudhui mbalimbali yanayoelekea kukiuka 'kanoni' katika vitabu vilivyoteuliwa ni kama vile.

## Maudhui ya Siasa za Kabla ya Uchaguzi Mkuu

Hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi* inahusu mgogoro kati ya Sungura na wanyama wenzake. Sungura alikuwa amesaidiwa na wanyama kuukwea mwembe kwa ahadi kuwa akifika juu ya mwembe angewaangushia wanyama wenzake maembe lakini alipoyafikia alikula peke yake bila

kuwaangushia wanyama hata embe moja. Mwanzoni mwa hadithi tunakutana na wanyama waliokusanyika chini ya mwembe kujadili na kuamua namna watakavyofikia matunda ambayo waliyaona juu ya mwembe. Mwembe ulikuwa na maembe mengi. Mengine yalikuwa yameiva na mengine yalikuwa mabichi. Wanyama walitamani sana yale yaliyokuwa yameiva. Tatizo kubwa walilokuwa nalo ni kuwa walikuwa na njaa na pili hawangeweza kufikia maembe waliyoyatamani kwa sababu yalikuwa juu ya mwembe ulikuwa mrefu na wenye utelezi.

Mnyama wa kwanza kutoa pendekezo la suluhisho alikuwa Fisi. Fisi alishauri kuwa watafute mawe walenge yale maembe mabivu na yakianguka wa kwanza kula awe ni yeye Fisi. Fisi, hata hivyo, hakufanikiwa kuangusha hata embe moja bivu kwa kutumia mawe badala yake yalianguka maembe mawili mabichi. Hapo ndipo Sungura anapoibuka na wazo kuwa wanyama watengeneze ngazi kisha wamshikie mmoja wao ili apande na akiwa juu awaangushie matunda yaliyoiva. Wanyama walikubaliana kwa kauli moja na wazo la Sungura. Fisi akauliza ni nani ambaye angekwea juu ya mwembe. Mara moja Sungura akasema angekwea yeye. Wanyama wengine walinung'unika lakini Sungura akaendelea kudai kuwa alikuwa amejitolea kuwasaidia. Baada ya kujadiliana wazo la Sungura, wanyama walikubaliana wamtengenezee Sungura ngazi na kisha wakamsaidia kuukwea ule mwembe kwa ahadi kuwa akifika juu hangewasahau na kwamba angewaangushia matunda. Sungura alitoa mwito wa umoja akisema kuwa kwa umoja wao wataweza kupata matunda. Sungura alikuwa mwenye maneno matamu na wanyama waliamini maneno yake. Wanyama walikubali wito wa Sungura ingawa shingo upande. Wanyama walishika ngazi wakaielekeza juu ya mwembe na kumsaidia Sungura kupanda kwa kuishikilia ngazi isianguke. Wakati huo katika akili yake, Sungura aliwaona wale wanyama wakiwa wajinga sana kwa vile walifikiri anahatarisha maisha yake kwa ajili yao. Lakini wanyama hawakujua Sungura alikuwa akiwahadaa.

Sungura alipofika juu ya mwembe hakutimiza ahadi aliyotoa ya kuwaangushia wenzake matunda. Aliruka kwenye tawi lililokuwa na maembe mengi na akaendelea kula yale yaliyoiva bila kuwajali wale wanyama waliokuwa wanamwangalia kwa macho ya njaa wakiwa chini. Sungura aliendelea kula maembe peke yake. Alianza kwa kula yale yaliyokuwa mabivu na kisha yale yaliyokuwa mabichi bila kuwajali wanyama wenzake waliokuwa na njaa chini ya mwembe na ambao walikuwa wamemsaidia kufikia maembe yale. Aliangusha maganda ya matunda bila kuwaangushia hata tunda moja. Wanyama waliendelea kungojea awaangushie maembe kutoka mtini. Walisubiri chini wakiwa na matumaini kuwa atawaonea huruma. Sungura aliendelea kula maembe raha mstarehe kama Rais kwenye Ikulu huku matumbo ya wanyama yakiuma kutokana na njaa. Wanyama hao walikasirika kwa sababu Sungura aliwadharau ilhali wao ndio waliokuwa wamemwezesha kufika hapo juu penye maembe. Walilalamikia tabia ya Sungura ya unafiki.

Kwa msingi wa nadharia ya uhalisia kuegemea mhimili wake mkuu ambao ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii, uhusiano wa maudhui na matukio halisi katika jamii ya mwaandishi ambayo ni jamii ya kikenya, unaweza kudhihirika. Masuala mbalimbali ya kisiasa yanaendelezwa katika hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi* na *Urembo wa Ngiri*. Kwa kutumia mtazamo wa nadharia ya uhalisia tukiegemea mhimili wake mkuu ambao ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii tunapata kwamba masuala hayo ya kisiasa yanahusiana na hali halisi katika jamii ya nchi ya Kenya. Masuala ya kisiasa yanayochochea maudhui katika hadithi hizi mbili yana uhusiano mkubwa na uchaguzi mkuu nchini Kenya ambako ndiko mwaandishi wa hadithi anakoishi. Masuala haya yanaweza kuchunguzwa katika vitengo viwili. Kuna masuala yanayohusu matukio ambayo yanashuhudiwa kabla ya uchaguzi na yale yanayohusu matukio ya baada ya uchaguzi.

Kwa mtazamo huu, kisa cha *Sungura Mpanda Ngazi* kinaweza kulinganishwa na kipindi cha kampeni nchini Kenya ambapo wanaowania nyadhifa mbalimbali hutumia kipindi cha

kampeni kujitetea kwa kutoa ahadi kuhusu mambo watakayowatimizia wapiga kura. Ahadi nyingi huishia kuwa za uongo kwa kuwa wanapochaguliwa husahau ahadi walizotoa na kuanza kujishughulisha na mambo ya kujitajirisha wao wenyewe huku wakisahau watu waliowachagua. Suala la ubinafsi pia linajitokeza kupitia mhsika Sungura. Tabia hii pia inaweza kulinganishwa na viongozi wanaowania nyadhifa za uongozi huku wakiweka mikataba ya makubaliano na wenzao halafu wanapokalia viti wanatupilia mbali mikataba hiyo na kuwapuuza hao wenzao.

## Maudhui ya Siasa za Baada ya Uchaguzi Mkuu

Hadithi ya *Urembo wa Ngiri* inahusu matukio ya baada ya uchaguzi mkuu. Katika hadithi hii mgogoro unawakumba wanyama nyikani kutokana na mashindano ya urembo waliyofanya kisha wakakosa kukubaliana ni nani hasa aliyeshinda. Kulingana na matokeo yaliyotangazwa chui ndiye aliyeshika mkia. Hakuamini. Alipinga matokeo hayo na kudai kuwa alinyang'anywa ushindi. Akadai kuwa kura zake zimeibiwa. Chui alikataa kutambua ushindi wa Ngiri. Vita vilizuka baina ya wafuasi wa Chui na wafuasi wa Ngiri. Chui alichochea wafuasi wake kuchoma makazi ya Ngiri ili kumfukuza nyikani. Wanyama wenye madoadoa waliwafukuza wale wasio na madoadoa nyikani. Ilimbidi Ngiri ahamie msituni pamoja na wanawe na kuishi kama mkimbizi. Mwishoni mwa hadithi hii safari ya maridhiano inaanza.

Hadithi ya *Urembo wa Ngiri* kwa upande wake, ina uhusiano wa karibu sana na hali iliyokumba nchi ya Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007. Baada ya matokeo ya uchaguzi huo kutangazwa, mzozo ulizuka kuhusu ni nani aliyeshinda uchaguzi wa Urais huku upande ulioshindwa ukikataa matokeo na kudai kuwa wamenyang'anywa ushindi. Kulingana na Kriegler na Waki (2009), kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Urais tarehe 30 Desemba 2007 ghasia zilizuka katika maeneo mbalimbali nchini Kenya kukiwa na madai kuwa Tume ya Uchaguzi ya Kenya – ECK – ilikuwa imetumia udanganyifu katika uchaguzi wa Urais. Sawa na ripoti ya Kriegler na Waki (2009), FIDA – K (2008) ilieleza kuwa Kenya ilifanya Uchaguzi Mkuu Desemba 27, 2007 ambao matokeo yake yaliyotangazwa tarehe 30 mwezi huo yalizua ghasia za ghafla wakati viongozi wa upinzani walioshindwa walipokataa matokeo yaliyotangazwa.

Visa hivi viwili vimefungua ukurasa mpya katika fasihi ya watoto na kuipa uhai zaidi kwa kuzungumzia masuala halisi ya kisiasa. Hadithi kama hizi ni ukiushi wa 'kanoni' kwa kuwa haikuwa kawaida kuzungumzia masuala kama haya katika fasihi ya watoto. Hata hivyo zinafaa kwa kuwa zaweza kuchochea watoto kuanza kuwazia na kuelewa mielekeo ifaayo na ile isiyofaa kuhusiana na masuala ya kisiasa.

## Maudhui ya Upelelezi

Katika hadithi ya *Kijana Mpelelezi*, mwaandishi amekiuka 'kanoni' kwa kuingiza maudhui ya upelelezi katika fasihi ya watoto. Katika kisa hiki Kangwana na Maria wanaalikwa na shangazi yao kumtembelea wakati wa likizo. Wanapofika huko wanakumbana na mambo mengi kuihusu nyumba ya shangazi. Kangwana, ambaye ana umri mkubwa zaidi ya wenzake, anaamua kufanya uchunguzi kuihusu nyumba hiyo ili kugundua siri iliyokuwa imefichwa miaka mingi. Kisa hiki kinaelekea kufungua ukurasa mpya katika fasihi ya watoto kwa kuingiza upelelezi katika fasihi hii jinsi mwandshi Mohammed Said Addulla alivoingiza upelelezi katika fasihi ya watu wazima kwa vitabu vyake kama vile *Siri ya Sifuri* na *Kisima cha Giningi*. Watoto wanaweza kufurahia ukakamavu wa mhusika mkuu katika hadithi hii na kukuza ujasiri wao. Maudhui haya ya upelelezi yaelekea kuleta na mvuto wa kipekee katika fasihi ya watoto.

## Fani Zinazotumika kuficha Ukiushi wa Kimaudhui

Maudhui ya kisiasa yameweza kufichwa kwa njia mbalimbali katika hadithi za *Sungura Mpanda Ngazi* na *Urembo wa Ngiri* ili kuzifanya hadithi hizi kusalia katika kitengo cha fasihi ya watoto. Licha ya kukiuka 'kanoni' kimaudhui, hadithi hizi zimezingatia sifa nyingi ambazo zinahusishwa na fasihi ya watoto na ambazo hufanya fasihi hii iwavutie watoto. Aghalabu, watoto huvutiwa na mambo tofauti na watu wazima. Tofauti na hadhira ya watu wazima huenda wasivutiwe na hata wasielewe masuala ya kisiasa yaliyowasilishwa katika hadithi. Wakati ambapo watu wazima wanaosoma hadithi hizi watayaona moja kwa moja masuala ya siasa za uchaguzi mkuu, huenda watoto wengi hata wasing'amue kuwa yapo masuala kama hayo. Sababu kubwa inatokana ufinyu wa tajriba ya watoto katika itikadi za kisiasa, uchanga wa urazini wao pamoja na mbinu alizotumia mwaandishi kuwasilisha maudhui ya kisiasa kwa njia fiche. Mbinu mbalimbali za kiufundi zimetumika kwa ubunifu mkubwa. Mwaandishi wa hadithi zinazohusu siasa za uchaguzi mkuu ambazo ni *Sungura Mpanda Ngazi* na *Urembo wa Ngiri* ametumia ubunifu mkubwa ili kazi yake ibai? kuwa fasihi ya watoto. Amefanya hivi kwa kuzingatia sifa nyinginezo za fasihi hii kama vile:

## Picha

Matumizi ya picha kwa wingi yamefanya hadithi hizi zisalie katika fashi ya watoto licha ya kuwa zina maudhi ya kisiasa. Picha katika hadithi ni sifa muhimu katika fasihi hii. Kwa kawaida mtoto anapopewa kitabu cha hadithi kusoma, huanza kwa kuangalia kama kuna picha za kuvutia huku akiangalia urefu wa kitabu. Kisipokuwa na picha kitamchosha na atakiweka chini. Kutokana na wingi wa picha, kinachomjia mtoto akilini haraka akiona picha hizi ni kuwa hadithi hii inahusu wanyama wala si binadamu. *Sungura Mpanda Ngazi* kimejaa picha za wanyama. Picha hizo ni kama vile wanyama wanaotazama maembe wakiwa chini ya mti ukurasa wa 2, fisi akilenga kuangusha maembe kwa kuyatupia mawe ukurasa wa 4, sungura akisaidiwa na wanyama wenzake kuupanda mwembe kwa kutumia ngazi katika ukurasa wa 10, sungura akila maembe raha mstarehe juu ya mti katika ukurasa wa 12 na 14 kati ya picha nyingine.

## Matumizi ya Wahusika Wanyama

Sifa nyingine inayohusishwa na fasihi ya watoto na ambayo imefanya hadithi hizi kubaki katika fasihi ya watoto ni matumizi ya wahusika wanyama. Wahusika wanyama kama vile Sungura ambaye ndiye mhusika mkuu katika *Sungura Mpanda Ngazi* na wanyama kama vile Ngiri na Chui ambao ni wahusika wakuu katika *Urembo wa Ngiri* yanasawiri hadithi hizi kama hurafa tu za burudani kwa mtoto. Maoni ya makala hii ni kuwa watoto wengi wa umri unaokusudiwa kusoma hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi* wakiona sungura akisaidiwa na wanyama wenzake kupanda mti katika ukurasa wa 10 na sungura akiwa anakula matunda akiwa juu ya mti katika ukurasa wa 12 wataona tu mnyama aliyetumia ujanja kujipatia matunda baada ya kuwadanganya wanyama wenzake wamsaidie kuukwea mwembe. Mtoto kama huyo atachangamka kumwona Sungura juu ya mwembe akiyala maembe. Pengine atawahurumia wanyama waliobaki chini ya mti wakimtazama Sungura huku matumbo yao yakiwa na njaa. Labda watoto watamwona Sungura kama mnyama asiye mzuri kutokana na udanganyifu wake lakini hawataweza kung'amua moja kwa moja kuwa kuna wanasiasa wenye tabia kama zile. Hii ni kwa sababu wanasiasa wanaofanya kampeni ili waweze kuchaguliwa kwenye nyadhifa wazitakazo ni watu wazima na ambao mtoto haelewi vizuri mbinu wanazotumia kujitafutia kura na ushindi.

Hivyo basi, kwa watoto wengi hadithi hii kikawaida itaishia katika kutoa mafunzo kwa mtoto hasa kuwa yeye asijekuwa na tabia kama zile za Sungura wala haitamzindua kufikiria uchaguzi mkuu ila pengine baada ya kufafanuliwa kisa kile na watu wazima waliosoma ile

hadithi kamma vile walimu. Akifafanuliwa atapata mafunzo zaidi kemkem na pengine kuelewa siasa za nchi yake zinavyoendeshwa. Uelewa huu waweza kuwa chanzo cha kuchukua mielekeyo ifaafayo ya kisiasa katika akili yake anapoendelea kukua.

Matumizi ya wanyama kama vile Ngiri na Chui katika *Urembo wa Ngiri* yamefanya hadithi hii kumvutia mtoto kuisoma bila kuwa na hisia nzito zinazoweza kusababishwa na kule kusoma kuhusu vita vikali baina ya makundi ya watu yanayozozana katika jamii. Kusoma kuhusu kuuawa kwa wanyama na kuchomwa kwa makazi yao kunapunguza makali ya vita ikilinganishwa na kuuawa kwa watu na kuchomewa nyumba zao. Kwa mfano mhusika mkuu anapopata shida kubwa hisia za huruma huchochewa moyoni mwa mtoto msomaji kwa mfano katika hadithi ya *Urembo wa Ngiri* ukurasa wa 51 watoto wa Ngiri wanauliwa na chui. Tunaaambiwa:

> *'Kila mara watoto wa Ngiri walipojaribu kutoroka walikutana na panga iliyotiwa makali. Chui aliwachinja watoto wawili wa Ngiri bila huruma. Damu ya wana wa Ngiri ilitririka ikawa mto wa damu. Chui aliwauwa wawototo wawili wa Ngiri kwa kuwakatakata kwa panga. … watoto wengine wawili wa Ngiri walichomwa kwenye kichaka.'*

Mtoto msomaji anaposoma haya huhisi huruma juu ya yule mhusika anayeyeteswa. Ni maoni ya utafiti huu kuwa mtoto msomaji angeshikwa na huruma zaidi ingekuwa wanaoteswa ni watoto wa binadamu halisi kama ilivyokuwa katika ghasia za baada ya uchaguzi mkuu. Kwa kutumia wahusika wanyama, mwaandishi ameweza kupunguza makali ya hisia nzito za huruma.

### Matumizi ya Jazanda na Taashira

Jazanda ni picha inayosawiriwa akilini na mwandishi na ambayo inaweza kulinganishwa na hali halisi katika jamii. Kwa mfano, katika *Urembo wa Ngiri*, jazanda ya usiku wa manane na giza imetumika. Mifano ya jazanda hizi ni katika ukurasa wa 24 hadi ukurasa wa 26 ambapo tunaelezwa kuwa:

> *'Ikafika usiku wa manane… Chui akaja ukumbini kutoka msituni … alirusha kiti … waamuzi wagongwa vichwani.'*

Katika ukurasa wa 25 tunaelezewa kuwa mnyama mwingine kwa jina Kicheche alizima taa. Giza lilipotanda kote ukumbini, viti vilivyokuwa vimekaliwa na wanyama vilitumiwa kama zana za vita. Chui alisikika akitoa vitisho kuwa:

> *'Hakutakuwa na amani kama sitakabidhiwa ushindi.'* (ukurasa wa 26).

Baada ya maneno haya ghasia zilizuka usiku wa manane kukiwa na giza nene. Taa zilizimwa na wanyama wakaanza kuwashambulia wengine. Kuzimwa kwa taa kunaashiria mwanzo wa maovu.

Katika *Urembo wa Ngiri*, mashindano ya urembo ni jazanda kwa kuwa yanaweza kulinganishwa na mashindano ya kisiasa ambayo huweko na ushindani wa ni mwanasiasa yupi mwenye kupendeza watu wengi kuliko mwingine au ni nani aliye mashuhuri kuliko mwingine. Baada baada ya kujitetea katika kumbi na majukwaa ya kisiasa katika shughuli za kampeni hatimaye wao hukutana kwenye uchaguzi ambapo kura hupigwa ili kuamua ni nani anayependwa mzuri zaidi ya wengine. Kutokana na tajriba yake, mtoto anayesoma kwa hakika

atakuwa anaona kisa kinachohusu mashindano ya urembo bila kuweza kuyaambatanisha na hali halisi ya kisiasa nchini. Kwa hivyo, mwaandishi amjificha katika mashindano hayo kuwasilisha masuala ya kisiasa kwa njia inayomchangmsha mtoto. Hadithi hii inafaulu kubakia katika kategoria ya fasihi ya watoto kutokana na kutimizwa kwa sifa nyingi zinazafiki fasihi ya watoto. Masuala ya ghasia za baada ya uchaguzi mkuu ambayo yanahusu watu wazima wenye kupiga na kupigiwa kura za nyadhifa za uongozi nchini hayajitokezi kwa njia ya moja kwa moja kwa mtoto.

Jazanda inapatikana pia katika nambari zinazotajwa katika *Urembo wa Ngiri*. Mathalani, wanyama sita walionyesha urembo wao jukwaani. Uamuzi wa kutumia nambari *sita* kuwa idadi ya wanyama walioshindana, unaweza kulinganishwa na kusemwa kuwa umetokana umuhimu wa nambari hii katika siasa za uchaguzi mkuu nchini. Kutokana na utafiti huu nambari sita ina umuhimu mkubwa katika siasa za Kenya kwa kuwa sita ni sawa na idadi ya nyadhifa za uchaguzi mkuu nchini Kenya ulioanza kufanyika baada ya katiba ya 2010 kutekelezwa. Nyadhifa hizo sita ni: Urais, Ugavana, Useneta, Ubunge, Uwakilishi wa Wadi na Uwakilishi wa wanawake. Hata hivyo, kwa mtoto asiyekuwa na habari za uchaguzi mkuu na maelezo ya ni nambari gani zinazohusiana nao, atachangamkia hadithi jinsi ilivyo kwamba ni kuhusu mashindano ya urembo ya wanyama ambapo vita vilitokea baada ya baadhi ya wanyama kukataa kukubali ushindi wa Ngiri.

Maudhui ya upelelezi yamefichika kwa kutumia jazanda ya nyumba ya shangazi. Kinachobainika kwa mtoto ni mambo ya nyumbani tu lakini ni vigumu kuyahusisha na mambo ya eneo pana kama jamii au nchi nzima.

## Hitimisho

**Makala hii imebainisha** kuwa fasihi ya watoto inayoandikwa na kizazi kipya inadhihirisha ukiushi wa 'kanoni' ya maudhui. Aina mbalimbali za ukiushi wa 'kanoni' kimaudhui zinazodhihirika katika vitabu teule vya fasihi ya watoto vilivyochunguzwa katika makala hii ambavyo ni *Sungura Mpanda Ngazi*, *Urembo wa Ngiri* na *Kijana Mpelelezi*. Imebainika kuwa licha ya ukiushi huu, kazi zile bado zimebaki katika kitengo cha fasihi ya watoto kutokana na fani alizotumia mwaandishi kuficha ukiushi ulio wazi kwa kuzingatia sifa nyingine za fasihi hii. Ukiushi huu unaelekea kuzua mgogoro mpya kuhusu iwapo fasihi ya watoto izingatie 'kanoni' za kimapokeo au iandikwe kwa njia huru kutegemea ubunifu wa mwandishi.

## Marejeleo

Bakize, L.H. (2014) *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bhroin C. & Patricia Kennon (2012) *What do we tell the children. Critical essays on children literature*. Cambridge Scholars Publishing.

FIDA- K. (2008) *Tume ya Kitaifa ya Upatanishi na Maridhiano*. Nairobi. Fida Kenya.

Hunt, P. (2002) *Understanding children's literature*. London: Routledge, Taylor & Francis e-library.

KICD (2017) *Basic Education Curriculum Framework*. Nairobi: KICD.

Kobia, J. (2008) *Sungura Mpanda Ngazi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kobia, J. (2016) *Urembo wa Ngiri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kriegler na Waki (2009) *Reports on 2007 Elections*. Nairororobi: Primark Ventures.

Lundin, A. (2004) *Constructing Canon in Children's literature*. New York & London: Routledge.

Ngugi, P.M.Y. (2012) "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati." Katika: S. Omari na G. Mrikaria (wh) *Mulika*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Na. 31. 2012 12 - 26

Omolo, L.O. (1968) *Mtaka Yote Hukosa Yote*. Nairobi: Longhorn.

Omolo, L.O. (1971) *Mikasa ya Joseph Juma*. Nairobi: Longhorn.

Somba, J.N. (1968) *Kuishi Kwingi ni Kuona Mengi*. Nairobi: East African Publishing House.

Somba, J.N. (1969) *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Swingewood, A. (1975) *The Novel and Revolution.* London: The Macmillan Press Ltd.

Wamitila, K.W. (2007) *Kijana Mpelelezi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.

Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.